TANGAZO LA SERIKALI Na. 865 la tarehe. 18/10/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MAEGESHO NA VITUO VYA VYOMBO VYA USAFIRI YA HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 209 la 2024

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga ya Mwaka 2024, ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”

Marekebisho ya kanuni ya 7

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 7(3) kwa kuongeza maneno “isipokuwa katika hali ya dharura” mara baada ya neno “umma”.

Marekebisho ya kanuni ya 9

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 9(3), kwa-

(a) kuongeza maneno “isipokuwa kama uharibifu huo utasababishwa na mtumishi au wakala wa Halmashauri” mara baada ya neno “huo”; na

(b) kufuta alama ya nukta mara baada ya neno “huo” na badala yake kuweka alama ya mkato.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**4**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) kwa kufuta kipengele cha 2 cha sehemu (b); na

(b) katika kipengele cha 13 cha Sehemu A kwa kuongeza maneno "kwa siku" baada ya kiasi "10,000/=".

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*